**NENO LA UKARIBISHO LA MTENDAJI MKUU WA WAKALA YA SERIKALI MTANDAO, DR. JABIRI KUWE BAKARI KWENYE UFUNGUZI WA KONGAMANO LA KWANZA LA SERIKALI MTANDAO KATIKA UKUMBI WA AICC ARUSHA, TAREHE 19 AGOSTI, 2015**

***Mheshimiwa Balozi Ombeni Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi;***
***Mheshimiwa Daudi Felix Ntibenda, Mkuu wa Mkoa wa Arusha;***
***Ndugu HAB Mkwizu, Kaimu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;***
***Ndugu Makatibu Wakuu mliopo;***
***Ndugu Naibu Makatibu Wakuu mliopo hapa;***
***Ndugu Makatibu Tawala wa Mikoa mliopo;***
***Ndugu Watendaji wa Wakuu wa Taasisi za Umma;***
***Ndugu Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wakala ya Serikali Mtandao;***
***Watoa Mada;***
***Wageni Waalikwa;***
***Wana Habari;***
***Mabibi na mabwana;***
***Itifaki imezingatiwa.***

***Habari za asubuhi.***

Kwa heshima na taadhima, nachukua fursa hii kukukaribisha rasmi wewe mgeni rasmi pamoja na washiriki wote wa Kongamano la Kwanza la Serikali Mtandao linalofanyika kwenye ukumbi huu hapa mkoani Arusha.

***Ndugu Mgeni Rasmi na Washiriki***

Hili ni Kongamano la Kwanza la Serikali Mtandao kufanyika hapa nchini. Kwa mwaka huu. Awamu ya kwanza iliyomalizika jana ilikuwa na washiriki 527. Awamu ya pili inategemewa kuwa na washiriki wasiopungua 200 wengi wao wakiwa maafisa masuhuli. Kundi la kwanza lilihusisha watendaji wanaohusika na TEHAMA, Mawasiliano, Mipango, Utawala na Rasilimaliwatu kutoka kwenye taasisi za umma. Awamu hii ilimalizika jana baada ya kuendelea kwa siku mbili kuanzia tarehe 17 hadi 18. Hili ni Kundi la pili linalowashirikisha Makatibu Wakuu na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Serikali na viongozi wengine katika ngazi ya maamuzi ambalo linakutana leo tarehe 19 na 20, Agosti 2015.

Aidha, watalaamu wawili kutoka India na Singapore wamekaribishwa ili kubadilishana uzoefu wao na washiriki wa Kongamano hili. Karibuni sana Dr. Rajendra Kumar Dr. Rajendra Kumar, Ex-Joint Secretary (e-Gov), Department of Electronics and Information Technology, Government of India na Bw. TAN Kim Leng – Managing Director, KDi Asia Pte Ltd. Karibuni sana. Ushiriki na mwaliko wa wajumbe wa Kongamano hili pamoja na watalaamu hawa umezingatia nafasi, mchango, uzoefu na umuhimu wa kila mshiriki katika utekelezaji wa Serikali Mtandao.

***Ndugu Mgeni Rasmi***

Mada zitakazowasilishwa katika mkutano huu zitajikita katika maeneo makubwa matano ya Serikali Mtandao ambayo ni Usimamizi na Utekelezaji wa Serikali Mtandao, Hali ya Miundombinu ya Serikali Mtandao, Utekelezaji wa Mpango wa Uendeshaji wa Serikali kwa Uwazi na Mfumo wa Takwimu Huria nchini, Huduma

za Serikali kupitia simu za mkononi pamoja na mifumo inayotumika kutoa huduma kwa Wananchi.

***Ndugu Mgeni Rasmi na Washiriki,***

Kaulimbiu ya Mkutano huu ni; ***"Kuelekea Matumizi ya Rasilimali TEHAMA Zilizowianishwa katika kutoa Huduma Bora kwa Umma.*** *(**Towards Harmonized ICT Recourses for Improved Public Services Delivery**)".* Falsafa ya Kaulimbiu hii ni kuhamasishana, kukubaliana na hatimaye kuwa na uelewa mmoja miongoni mwa taasisi za umma katika kuhakisha kunakuwepo na uwekezaji wenye tija wakati wa usimikaji na matumizi ya miundombinu na mifumo ya TEHAMA. Lengo ni kuziwezesha taasisi hizo kushirikiana katika matumizi ya rasilimali za TEHAMA ili kuondoa urudufu, kupunguza gharama na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma na kuhakikisha usalama wa mawasiliano. Matumizi ya rasilimali TEHAMA ziliooanishwa utawezesha ubadilishanaji wa taarifa miongoni mwa taasisi za Serikali, hivyo kutoa fursa kwa matumizi ya TEHAMA yatakayorahisisha mawasiliano na utangamano (integration) wa mifumo mbalimbali. Hali hii itaweza pia kurahisisha ukusanyaji, uhifadhi, utumiaji, uhuishaji na ubadilishanaji wa taarifa miongoni mwa taasisi na sekta zote za umma.

Dhima ya Kongamano hili ni kujenga uwezo na ushirikiano katika kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma pamoja na kuwaleta pamoja wadau wakuu wa Serikali Mtandao kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazokabili utekelezaji wa Serikali Mtandao hapa nchini. Mkutano huu pia umelenga kuwawezesha washiriki kuongeza ufahamu, kubadilishana uzoefu, kushirikiana na kukuza uhusiano wa kikazi na wataalam wanaohusika na Serikali

Mtandao kutoka nchi zinazofanya vizuri katika eneo la Serikali Mtandao hususani nchi za India na Singapore.

***Ndugu Mgeni Rasmi,***

Kipekee nichukue fursa hii kutoa shukrani za pekee kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa msaada wa hali na mali uliowezesha kufanikisha Kongamano hili muhimu. Mwisho japo si kwa umuhimu, naomba nitambue michango ya hali na mali kutoka kwa wadau wetu wote waliowezesha Kongamano hili kufanyika. Wadau hao ni taasisi za Serikali zilizoweza kuchangia na kuleta wawakilishi wao kwenye mkutano huu pamoja na Taasisi za TASAF, TCRA, NHIF, na Kampuni za COMPUTECH, COPY CATS na ZANTEL. Sisi kama Wakala, tunasema Ahsanteni sana.

Baada ya kusema haya machache naomba namkaribisha mratibu wa shughuli hii aendelee na ratiba.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**